

## **HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**



### **TANGAZO**

30/08/2023

### **ZABUNI YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA NJE (OPD COMPLEX) KATIKA HOSPITALI YA JIJI ARUSHA**

### **ZABUNI NA. LGA/003/2023/2024/W/**

Halmashauri ya Jiji la Arusha inawatangazia wananchi wote kuwa inatafuta LOCAL FUNDI wa kazi za ujenzi OPD Complex – Hospitali ya Jiji Arusha Kwa kazi zifuatazo:-

1. FOAM WORK
2. UJENZI WA TOFALI
3. KAZI ZA KUWEKA VYUMA
4. KAZI ZA MFUMO WA UMEME
5. KAZI ZA MFUMO WA MAJI SAFI NA MAJI TAKA
6. KAZI ZA UMALIZIAJI (RANGI + UWEKAJI WA VIGAE)

#### **Sifa na Vigezo vya fundi anayetakiwa:**

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe na uzoefu wa kujenga majengo ya serikali / binafsi au mashirika kwa kiwango cha juu
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri michoro mbalimbali ya ujenzi (ramani) na kuielewa
4. Awe na uwezo wa kusoma BOQ
5. Awe na uwezo wa kuandaa gharama za ujenzi kuanzia Uandaaji wa eneo , msingi hadi umaliziaji
6. Awe na namba ya uandikishaji wa mlipakodi toka mamlaka ya Mapato Tanzania ( Tax Identification Number) (Kama hana TIN namba aambatanishe kitambulisho cha NIDA au Namba ya NIDA)

7. Awe na akaunti benki au Awe na uwezo wa kufungua akaunti benki baada ya kupata zabuni
8. Fundi wa umeme awe na cheti cha ufundi umeme toka chuo kinachotambuliwa na serikali

### Masharti ya kazi

- (i) Maombi ya zabuni yaambatanishwe na nakala ya malipo ya Tsh. 50,000/= (Elfuhamsini tu) kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyopo katika Benki ya NMB tawi la Clock Tower, Akaunti na. **40801200336** baada ya kupatiwa control number ya malipo na kuwasilisha nakala ya hati ya malipo ya Benki (Bank Pay in slip Original) na kupata stakabadhi ya halmashauri kwa zabuni iliyombwa. Malipo yaliyotolewa kwa ajili ya maombi hayo ya zabuni hayatarejeshwa
- (ii) Fundi aombe kazi iliyotangazwa katika tangazo hili na Fundi anaruhusiwa kuomba Zaidi ya kazi moja
- (iii) Fundi atakayepata kazi, atatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri kupitia Mganga Mfawidhi – Hospitali ya Jiji Arusha kabla ya kuanza kazi
- (iv) Fundi anatakiwa kujaza fomu maalumu ya gharama za ufundi wa kujenga jengo husika hatua kwa hatua
- (v) Vifaa vyote vya ujenzi vitanunuliwa na kamati za mradi husika
- (vi) Ramani ya ujenzi pamoja na BOQ zinapatikana katika ofisi ya manunuzi na ugavi Halmshauri ya jiji la Arusha, chumba Na. 48
- (vii) Malipo yote yatafanyika kwa awamu baada ya kazi kukaguliwa katika hatua husika na wataalamu wa ujenzi na kutoa hati ya malipo (Interim Payment Certificate)
- (viii) Malipo yote ya fundi yatakatwa fedha za uangalizi ya asilimia tano (5%) pamoja na service levy asilimia 0.3%
- (ix) Mafundi wote watakaoomba kazi hii wawepo siku ya ufunguzi ili kujidhihirisha kwa taarifa zote zilizowasilishwa katika maombi
- (x) **Maombi yote yatumwe kwa Mganga Mfawidhi – Hospitali ya Jiji la Arusha – Njiro (Block D) , S.L.P 3013, ARUSHA**
- (xi) Maombi yote yafungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri (seal) na juu ya bahasha iandikwe “Zabuni ya fundi” (Local Fundi) NA. LGA . 003/2023/2024/W/ kulingana na kazi ya uliyoomba, Zabuni zitafunguliwa Tarehe 07/ 09 / 2023 siku ya Alhamisi saa nne na nusu asubuhi.
- (xii) Fundi awe na vifaa na mashine ndogo ndogo zinazohitajika kwa kazi husika , au awe na sehemu ambayo anaweza kuviazima

Wote mnakaribishwa

---

MGANGA MFAWIDHI  
HOSPITALI YA JIJI ARUSHA